MWANZA URBAN WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY
MWAUWASA

# MWAUWASA

## NEWS BULLETIN

MWAUWASA 2024 MWAUWASA 2024 MWAUWASA 2024 MWAUWASA 2024 MWAUWASA 2024










Toleo la: 0007 | Julai - Disemba 2024

www.mwauwasa.go.tz

Piga Simu Bure **0800110023**




## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti:**
Neli Msuya

**Katibu:**
Vivien Temu

**Wajumbe:**
Dioniz Kidai, Hadija Mabula
Jonas Christopher, Judith Mtui

**Msanifu Kurasa:**
Philipo Abdon Baraka | +255 678 434 236

# YALIYOMO











**01** WAZIRI MKUU AKAGUA MAENDELEO YA MRADI WA UJENZI WA TENKI LA MAJI KISESA - MAGU

**03** AWESO NA MIKAKATI YA MATUMIZI YA TEKNOLOJIA SULUHU YA UPOTEVU WA MAJI NCHINI

**04** MRADI MPYA NGUDU KUIMARISHA UPATIKANAJI WA HUDUMA YA MAJI KWA WANANCHI (DC KWIMBA AIPONGEZA WIZARA YA MAJI)

**06** AWESO AKAMILISHA KAZI YA WIKI KWA SIKU 1 BUHONGWA, KAZI YAKAMILIKA USIKU

**07** NAIBU WAZIRI WIZARA YA MAJI, MHANDISI KUNDO KIKAONI NA WATUMISHI WA SEKTA YA MAJI MWANZA

**09** WAZIRI AWESO AFUNGUA MKUTANO WA WATAALAM SEKTA YA MAJI

**10** MWAUWASA KUENDELEA KUIMARISHA UHUSIANO NA WATEJA

**11** MD MWAUWASA AFANYA ZIARA BUGANDA - MKOLANI

**12** ZAIDI YA KAYA 200 KUNUFAIKA NA MRADI MPYA WA MAJI IGOMBE – MWANZA

**14** MWAUWASA YASHIRIKI KIKAO CHA WANANCHI MTAA WA NG'WASHI

**15** MABORESHO MIUNDOMBINU YA MAJI BUHONGWA MAGHARIBI

**16** WATUMISHI MWAUWASA WANOLEWA

17 RC MTANDA AISIFU MWAUWASA KWA UTEKELEZAJI WA MIRADI INAYOENDELEA

18 MRADI WA MAJI KISIWA CHE BEZI KUNUFAISHA WANANCHI 6378

19 SERIKALI KUWEZESHA UPANUZI WA MRADI WA MAJI BUTIMBA AWAMU YA PILI

20 MBUNGE WA ILEMELA DKT. MABULA AZURU BANDA LA MWAUWASA NANENANE 2024

21 AGIZO LA NAIBU WAZIRI WA MAJI STONE TOWN – BUSWELU LATEKELEZWA KWA WAKATI

23 UWT YASIFU UTEKELEZAJI MRADI WA MAJI BUTIMBA

24 MWAUWASA YASHIRIKI KONGAMANO LA TATU LA KITAALUMA LA CHAMA CHA MADEREVA WA SERIKALI

25 ZAHANATI YA BULALE KATA YA BUHONGWA YAKUMBUKWA

26 MWAUWASA YAIBUA TABASAMU KWA WAKAZI WA NANSIO - UKEREWE

27 MRADI WA DHARURA SAHWA- BUHONGWA MBIONI KUKAMILIKA

29 MD MWAUWASA AWATIA MOYO MAFUNDI WANAFUNZI

30 NAIBU KATIBU MKUU WIZARA YA MAJI AZINDUA KAMPENI “MWAUWASA MTAA KWA MTAA”

31 MWAUWASA YAIBUKA MSHINDI WA PILI FAINALI MAJICUP 2024

32 KAMATI YA UKAGUZI BODI YA MWAUWASA YATEMBELEA KANDA ZA MWAUWASA

33 VIONGOZI KATA YA IGOMA WATETA NA MWAUWASA

34 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI KUCHOCHEA KASI YA MAENDELEO MWANZA (WIZARA YA MAJI YAPONGEZWA)

35 MWAUWASA YASHIRIKI USAFI SOKO LA MBUGANI KUADHIMISHA WIKI YA USAFI WA MAZINGIRA

36 MWAUWASA NA VEI ZAUNGANISHA NGUVU, KUPAMBANA NA UPOTEVU WA MAJI

37 WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA YAANZA KWA KISHINDO MTAA KWA MTAA

38 KAMATI YA KUDUMU YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR YAUPA TIKI MRADI WA MAJI BUTIMBA

40 MWENGE WA UHURU WARIDHIA MIRADI YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA MWAUWASA

41 WAKAZI WA “IBANDA BUSISI” KATA YA KIRUMBA KUBORESHEWA HUDUMA YA MAJI

42 ELIMU YA USAFI WA MAZINGIRA SHULE YA MSINGI BUTIMBA B

43 ZIARA YA BODI YA WAKURUGENZI KUWASA

44 ZIARA YA WANAFUNZI MWAUWASA KUJIFUNZA KUHUSU UZALISHAJI MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA

45 JELA MIAKA MITANO KWA KUMJERUHI MTUMISHI WA MWAUWASA

46 MWAUWASA YAWANOA WANAFUNZI WA SHARA NA MWENGE KUHUSIANA NA USAFI WA MAZINGIRA

47 MWAUWASA NA NEMC KUSHIRIKIANA UHIFADHI WA MAZINGIRA

48 SEKTA YA MAJI MWANZA NA WIZARA WAJADILI UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KIMKAKATI

49 UKAGUZI MIUNDOMBINU YA MAJITAKA

# WAZIRI MKUU AKAGUA MAENDELEO YA MRADI WA UJENZI WA TENKI LA MAJI KISESA - MAGU

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amekagua Maendeleo ya ujenzi wa tenki la kuhifadhi maji la Kisesa ambalo utekelezaji wake sasa umefikia asilimia 93 ukitarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2025.

Mradi huo ambao ni mpango wa muda wa kati wa kuboresha huduma ya maji Mwanza, wa ujenzi wa tenki litakalohifadhi maji kwa ujazo wa Lita Milioni Tano (5,000,000) unatarajiwa kuhudumia wananchi 75,000 wa maeneo ya Kisesa Bujora, Igudija na sehemu za jirani na unafadhiliwa na Serikali ya Tanzania na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (France Development Agency) kwa gharama ya TZS Bilioni 3.54

Akizungumza na wananchi wa eneo la Kisesa baada ya kukagua mradi huo Mhe. Majaliwa amesema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya kazi kubwa ya utekelezaji wa miradi mikubwa inayowagusa wananchi moja kwa moja kwenye sekta za elimu, afya, maji, kilimo, uvuvi na barabara.







"Mhe Rais katika mpango wake aliweka msisitizo kuwa wananchi wapate huduma ya maji hadi vijijini, na alilazimika kuongeza bajeti ya Wizara hii ambayo sasa Waziri Aweso anaendelea kuisimamia"






Kwa upande wake, Waziri wa Maji Jumaa Aweso amesema kuwa wizara hiyo itaendelea kusimamia maagizo ya Rais Dkt. Samia ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji ya uhakika katika maeneo yao.

Akitoa taarifa ya mradi huo mbele ya Waziri Mkuu, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) Neli Msuya amesema kuwa Matenki mengine yatajengwa katika maeneo ya vilima vinavyozunguka Mji wa Mwanza ikiwemo Nyamazobe (lita milioni 10), Buhongwa (Lita milioni 5), Fumagila (Lita milioni 10) na Usagara (lita milioni 1). "Utekelezaji wa mradi huu wa thamani ya Tsh. Bilioni 49 umeanza na unatarajiwa kukamilika ndani ya miaka miwili (2) ifikapo Desemba 2026".

# AWESO NA MIKAKATI YA MATUMIZI YA TEKNOLOJIA SULUHU YA UPOTEVU WA MAJI NCHINI

SEOUL - KOREA



Waziri wa Maji Mhe Jumaa Hamidu Aweso(MB) amewasili Seoul nchini Korea Kusini kwa mualiko maalumu wa Benki ya Exim ya Korea na mfuko wa mashirikiano ya kiuchumi wa Korea (EDCF) ambapo anatarajia kukutana na Makamu wa Rais wa Benki hiyo tarehe 06 Desemba 2024 kujenga mashirikiano zaidi baada ya uwekezaji wa serikali ya Korea kusini katika miradi ya Maji Taka kwa Majiji ya Dar Es Salaam, Dodoma na Manispaa ya Iringa.

Waziri Aweso amepokelewa na mwenyeji wake Mheshimiwa Togolan Edriss Mavura, Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Korea Kusini.

Aidha Waziri Aweso akiwa Seoul Korea, ametembelea moja ya makampuni makubwa ya Teknolojia katika Sekta ya Maji ya nchini Korea ya Green Tech. Inc ambayo imefunga mfumo wa mita janja (Smart Water Managemant System) katika Manispaa 43 nchini humo pamoja na nchi nyingine,ili kujionea Teknolojia hiyo pamoja na kuona namna mfumo huo unavyofanya kazi.





Mradi huu utawezesha kupunguza upotevu wa Maji na kusimamia ubora na msukumo wa maji katika mfumo wote wa usambazaji kupitia mfumo maalumu wa mawasiliano.

# MRADI MPYA NGUDU KUIMARISHA UPATIKANAJI WA HUDUMA YA MAJI KWA WANANCHI

## DC KWIMBA AIPONGEZA WIZARA YA MAJI








amlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) imeanza utekelezaji wa mradi wa ufufuaji Visima Viwili na Uboreshaji wa Mtandao wa Maji kwa KM 4.5 unaolenga kunufaisha wakazi wa mji wa Ngudu Wilayani Kwimba kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji.

Akizungumza wakati wa zoezi la mapokezi ya Shehena ya kwanza ya bomba yenye urefu wa KM 1.5, Mkuu wa Wilaya ya Kwimba Mhe. Ng'wilabuzu Ludigija ameshukuru Serikali kupitia Wizara ya Maji kwa kutekeleza ahadi kwa wakati na kusimamia nia ya Mhe. Raisi ya kumtua mama ndoo ya maji kichwani.

"Tumekuwa na changamoto ya uchakavu wa bomba kuu linalosafirisha maji kutoka chanzo cha Ihelele na kuhudumia Mji huu na Wizara kupitia Mhe. Waziri Jumaa Aweso aliahidi kutafuta mbadala wa haraka kwa mpango wa muda mfupi, tunaona leo mmetekeleza na kazi imeanza, nawapongeza kwa kubuni mradi huu na nawasisitiza MWAUWASA mfanye kazi hii kwa bidii ili ikamilike kwa wakati ninawaamini". Amefafanua Mhe. Ludigija.



Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA Neli Msuya amesema Mradi huo utakaogharimu kiasi cha TZS Milioni Mia tatu (300,000,000.00) utawezesha uzalishaji maji kwa Lita 600,000 kwa siku kutoka katika Visima na kupunguza changamoto ya uhaba wa maji. Alisema kwa bomba la Maji linalotoa maji chanzo cha KASHWASA cha Ihelele linawezesha mji huo kupata lita 600,000 kwa siku wakati mahitaji halisi ni lita milioni 1.2 kwa siku.

Aidha, Mkurugenzi Neli ameshukuru Mbunge wa Jimbo la Kwimba Mhe. Shanif Mansoor kwa ushirikiano wake tangu hatua ya kubuni Mradi na kuongeza kuwa Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Februari 2025. "Fedha za utekelezaji wa mradi tayari tumepatiwa na Waziri na kazi iliyobaki ni ya utekelezaji,"alisisitiza.

Akieleza kazi zitakazotekelezwa katika Mradi huo, Meneja wa Miundombinu MWAUWASA Mha. Stanley Mwasawala amesema Mradi utajumuisha ulazaji wa bomba jipya la usafirishaji maji kutpka katika chanzo hadi kwenye matenki kwa urefu wa KM 4.5, Ufungaji wa Pampu 3 za kuzalisha na kusukuma maji, Ufufuaji wa Visima viwili eneo la Kiliaboya, pamoja na ukarabati wa miundombinu chakavu katika chanzo hicho kilichoanza kutumika tangu mwaka 1995.

# AWESO AKAMILISHA KAZI YA WIKI KWA SIKU 1 BUHONGWA, KAZI YAKAMILIKA USIKU

Waziri wa Maji Mhe Jumaa Aweso amehakikisha Kazi iliotakiwa kufanyika ndani ya wiki moja ya ukamilishaji wa Mradi wa Maji wa Buhongwa jijini Mwanza iliotakiwa kukamilishwa mpaka ijumaa inafanyika ndani ya siku moja kwa kuamua kuweka kambi na mafundi site mpaka saa sita usiku.

Mradi wa dharula Buhongwa umekamilika usiku na Maji rasmi yamefika hapa Buhongwa Centre na kazi itakayofuata ni kuunganisha kwa wananchi.



Awali Waziri Aweso ameshuhidia maunganisho ya bomba ya mwisho ya mradi wa Sahwa Buhongwa ambao unalenga kutatua changamoto katika maeneo ya Sahwa, Lwanhima na Buhongwa.

Mara baada ya bomba la mwisho kuunganishwa saa 4.15 usiku alielekea katika kituo cha kusukuma maji Sahwa ili kuwasha pump ya maji kwa lengo la kusafisha bomba hilo.

Usiku huo huo Waziri Aweso amewakabidhi wenyeviti wa serikali za mitaa za Sahwa chini na Semba mabomba kwa ajili ya kusogeza maji katika maeneo yao.



Mradi huu una gharama ya Tshs. Milioni 864.816. Mradi huu utanufaisha wakazi wa mitaa ya Sahwa ya chini, Sahwa ya juu, Buhongwa mashariki, Buhongwa magharibi, Buhongwa centre na Maliza.

Jumla ya vituo nane vya kuchota maji vitajengwa katika maeneo hayo na kunufaisha wananchi katika mitaa husika.



# NAIBU WAZIRI WIZARA YA MAJI, MHANDISI KUNDO KIKAONI NA WATUMISHI WA SEKTA YA MAJI MWANZA



Naibu Waziri wa Wizara ya maji Mhandisi Kundo Mathew ameanza ziara yake ya kikazi mkoani Mwanza kwa kuzungumza na Watumishi wa sekta ya maji mkoani humo ambapo amesisitiza kufanya kazi kwa umoja huku wakiweka mbele upendo miongoni mwao na uzalendo katika kuwatumikia wananchi.

Ameyasema hayo wakati wa kikao maalum na Wafanyakazi wa sekta hiyo kilichofanyika makao makuu ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) Majihouse Julai 24, 2024.

“Ni muhimu kuwa na mnyororo wa thamani utakaothamini kila mtumishi kwa kila kada ili kufikia malengo ya pamoja tunayojiwekea katika kuwahudumia wananchi" amesisitiza.

Mhandisi Kundo ameelekeza Viongozi na Watumishi wa sekta ya maji mkoani Mwanza kutekeleza majukumu yao ya kazi kwa uzalendo na weledi ili kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuhakikisha huduma ya maji inaimarika na kuwafikia wananchi wa Mkoa wa Mwanza kikamilifu.

Akizungumza katika kikao hicho Mhe. Kundo alisema Wizara ya Maji itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa vitendo ili kufanikisha maono ya Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo ya maji kichwani.



"Tekelezeni majukumu yenu na kuwa kioo cha Mhe Jumaa Aweso na kuakisi jitihada zake na hatimaye kuhakikisha huduma ya maji ndani ya mkoa wa wa mwanza'' inaimarika.

Kikao hicho kimehusisha Watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) mkoa wa Mwanza, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sengerema (SEUWASA) pamoja na Bodi ya maji Bonde la ziwa Victoria.

Naibu Waziri huyo anaendelea na ziara yake ya kikazi ya siku nne mkoani Mwanza iliyoanza Julai 24 na atahitimisha Julai 27, 2024.

# WAZIRI AWESO AFUNGUA MKUTANO WA WATAALAM SEKTA YA MAJI

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso amefungua Mkutano maalum wa Wataalam wa Utawala na rasilimali watu, Maafisa Maendeleo ya Jamii pamoja na Maafisa Mawasiliano na Uhusiano wa Sekta ya maji unaofanyika katika ukumbi wa NSSF Mafao House Jijini Dar es Salaam.






Mkutano huo maalum wa Mwaka unafanyika Kwa siku 3 kuanzia Novemba 14 hadi 16 ukiwakutanisha Wataalamu hao kutoka Sekta ya Maji nchini ukibeba Kaulimbiu isemayo " Rasilimali Watu ni chachu ya maendeleo endelevu katika sekta ya maji"

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mkutano huo wenye lengo la kuwakumbusha na kujengea uwezo wa masuala mbalimbali ya kiutendaji kwa Wataalam hao, Waziri Aweso amesisitiza kutambua nafasi na umuhimu wa kila Kada pamoja na kuendelea kufanya kazi kwa umoja, upendo na kuzingatia Weledi ili kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata huduma bora na muhimu ya maji na kutimiza dhamira ya Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo ya



# MWAUWASA KUENDELEA KUIMARISHA UHUSIANO NA WATEJA


Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) imetembela wateja wakubwa, Binafsi na Taasisi mbalimbali za Serikali kwa lengo la kuboresha huduma na kubaini changamoto zao na kubadilishana uzoefu ili kuongeza juhudi katika kuhudumia jamii.

Akizungumza wakati alipotembelea wateja katika kanda ya Nyakato, Meneja wa huduma kwa Wateja Bi. Sia Mrema ameeleza kuwa, lengo la Mamlaka ni kutoa huduma bora inayokidhi matarajio ya wateja.

Nae Kaimu Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano na uhusiano Vivien Temu ameeleza kwamba katika kuboresha huduma za mawasiliano ni suala la muhimu sana ikiwemo kupokea maoni, changamoto na hoja za wateja na kuzitolea majibu kwa wakati.

Kwa upande wake, ndugu Suresh Tripurari ambaye ni Meneja wa uendeshaji (Operation Manager) kutoka Kiwanda cha Pepsi ikiwa ni sehemu ya taasisi binafsi zilizotembelewa ameipongeza MWAUWASA na kutoa wito wa kuendelea kuboresha zaidi huduma kwa wateja kwa kuongeza wigo kwa wateja kutoa mrejesho wa huduma kwa Mamlaka ili kinapohitajika maboresho ya kihuduma yafanyie kwa wakati.

"Leo tumetembelea baadhi ya Taasisi za Serikali na binafsi zikiwemo Kiwanda cha Pepsi, Kiwanda cha Coca cola, chuo cha Mwanza na nyingine nyingi tumefurahi kuona wanaridhika na huduma zetu na wameahidi kuongeza ushirikiano ili kuboresha zaidi" amesema Bi. Sia



"Nimefurahi MWAUWASA kutembelea Taasisi yetu leo ni jitihada kubwa lakini bado kuna haja ya kutoa elimu zaidi kwa wateja haswa haki na wajibu wao kwa Mamlaka", amesema ndugu Suresh.

# MD MWAUWASA AFANYA ZIARA BUGANDA - MKOLANI

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) Ndugu, Neli Msuya ametembelea Mtaa wa Buganda Kata ya Mkolani kwa lengo la kukagua hali ya upatikanaji wa huduma ya maji na kuzungumza na viongozi wa mtaa kujadili hatua zinazochukuliwa na MWAUWASA katika kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji hususani kwa maeneo yenye changamoto ndani ya kata kiyo.



Amefanya ziara hiyo tarehe 04 Julai, 2024 akiwa ameambatana na Wataalam kutoka MWAUWASA.

“Nipo hapa Buganda kwa ajili ya kujiridhisha hali ya upatikanaji wa maji na pia kuzungumza na Viongozi wa Mtaa kuwaeleza namna ambavyo tumejipanga kupambana na changamoto ya upatikanaji wa huduma kwa awamu,” amesema Mkurugenzi Neli na kuongeza kuwa amekuwa na majadiliano mbalimbali na viongozi akiwemo Mbunge wa Nyamagana Mhe. Stanislaus Mabula.

Akizungumza katika kikao hicho, Neli Msuya amebainisha kwamba kazi inayoendelea kwa sasa ni kuboresha miundombinu kupitia miradi ya haraka, ya muda wa kati na miradi ya muda mrefu.

Ndugu Neli Msuya pia amewashukuru Viongozi wote kwa kuwasilisha maoni ya wananchi na kusema, Mamlaka imepokea na tayari inayafanyia kazi.

Naye Diwani Kata ya Mkolani Mhe. Dioniz Swalala ameshukuru kwa hatua za haraka za kupunguza tatizo la maji zilizochukuliwa na MWAUWASA.

“Uhitaji wa maji katika kata yetu ni mkubwa ila namna unavyoendelea kuwa na sisi bega kwa bega unatupa moyo pamoja na timu yako,” amesema Mhe. Swalala

Kama ilivyo ada, Mkurugenzi Neli hufanya ziara ili kutembelea mitaa mbalimbali kukagua mfumo wa usambazaji maji, hali ya upatikanaji wa huduma sambamba na kuzungumza na viongozi wa Mitaa ili kueleza hatua zinazochukuliwa na serikali.



# ZAIDI YA KAYA 200 KUNUFAIKA NA MRADI MPYA WA MAJI IGOMBE – MWANZA



Mkuu wa Wilaya ya Ilemela Mhe. Hasan Masala ameongoza wadau mbalimbali kujadili utekelezaji wa mradi mpya unaotekelezwa kwa ushirikiano baina ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) na Shirika la Maji la Uholanzi maarufu kama Vitens Evides Inter national (VEI).

Mkutano huo uliofanyika Julai 11, 2024 katika ukumbi wa mikutano (Majihouse), Wataalamu wameeleza kuwa Mradi umelenga kuboresha huduma ya majisafi, kwa kuunganisha kaya 200 zenye kipato cha chini kwa kata za Bugogwa, Nyamhongolo - Nyamadoke, Sangabuye - Nyafla, Shibula na Kahama, uboreshaji wa chanzo cha maji cha Igombe pamoja na ujenzi wa Magati 20 ambayo yatasaidia wananchi kupata huduma ya maji kwa uhaki ka. Mgeni Rasmi katika mkutano huo alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Mhe. Hassani Masala ambaye amepongeza jitihada za MWAUWASA kwa kushirikiana na VEI kwa kubuni mradi ambao utaimaimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa maeneo hayo.

“Pongezi ziende moja kwa moja kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha Sekta ya maji, kupitia jitihada zake za kuimarisha ushirikiano na uhusiano na wadau wa maendeleo wa kimataifa,” alisema Mhe. Masala.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Mhe. Dkt. Angelina Mabula aliishukuru Serikali kupitia Wizara ya Maji chini ya uongozi wa Mhe. Juma Aweso (Mb) kwa kuwezesha Mradi huo unaokwenda kutatua changamoto ya uhaba wa maji kwa wananchi kwa kunufaisha wakazi wapatao 34,014.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Ndugu Neli Msuya amewashukuru Wadau na washirika wa maendeleo kwa kufanikisha utekelezaji wa mradi huo utakaogharimu kiasi cha TZS 869,372,438.00 na kuomba ushirikiano huo uendelee wakati wote wa utekelezaji wa mradi kwa Wadau wote.

Kikao hicho kilishirikisha Madiwani wa kata husika, Wenyeviti wa Serikali za mitaa, Viongozi wa Manispaa ya Ilemela Wataalamu na wawakilishi wa wananchi wanufaika.



# MWAUWASA YASHIRIKI KIKAO CHA WANANCHI MTAA WA NG'WASHI

Wataalamu wa miundombinu na usambazaji maji kwa pamoja na Maafisa wa kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa MWAUWASA wameshiriki kikao cha Wananchi wa mtaa wa Ng'washi kata ya Buhongwa kwa lengo la kusikiliza na kupokea maoni ya wananchi na kujadili kwa pamoja kuhusu huduma ya maji kwa wakazi wa eneo hilo

Katika kikao hicho MWAUWASA imeeleza mipango iliyopo kuhusu uimarishaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa eneo hilo ikiwa ni pamoja na maboresho ya miundombinu ya usambazaji maji pamoja na ujenzi wa tenki la kuhifadhi na kusambaza maji katika eneo hilo litakalojengwa katika eneo la kagera.






Wananchi wa Ng'washi wameelezwa kuwa utekelezaji wa mipango hiyo unaanza mwezi Julai mwaka huu (ndani ya wiki ijayo) na kwamba MWAUWASA imejipanga kuhakikisha inaunga mkono dhamira ya Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo ya maji kichwani kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji.

Katika hatua nyingine, Wananchi wamekumbushwa kuendelea kuunga mkono juhudi hizo kwa kutoa ushirikiano kupitia utunzaji wa miundombinu ya maji, kutoa taarifa za hujuma (wizi) wa maji pamoja na kulipa ankara (bili) za maji kwa wakati ili kufanikisha utoaji wa huduma bora na endelevu.

# MABORESHO MIUNDOMBINU YA MAJI BUHONGWA MAGHARIBI

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) inaendelea na maboresho ya miundombinu katika eneo la Buhongwa Magharibi kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa eneo hilo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA akiambatana na timu ya Wataalamu ametembelea eneo hilo kukagua zoezi linaloendelea la kufumua mtandao wa bomba kwa kuondoa minyororo ya bomba na kuweka bomba mpya ili kuwezesha maji kuwafikia wakazi wa eneo hilo kwa ufanisi.



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA akiambatana na timu ya Wataalamu ametembelea eneo hilo kukagua zoezi linaloendelea la kufumua mtandao wa bomba kwa kuondoa minyororo ya bomba na kuweka bomba mpya ili kuwezesha maji kuwafikia wakazi wa eneo hilo kwa ufanisi.

Mkurugenzi Neli alikutana na kufanya mazungumzo na uongozi wa eneo hilo akiwemo Mwenyekiti wa Mtaa huo Ndugu Alfred Kimwaga na Balozi Ndugu Msemakweli Stan slaus Wote waliahidi kuendelea kushirikiana na Mwauwasa.



Maboresho hayo yanalenga kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa wakazi wa eneo hilo lenye vilima ambapo hapo awali hawakua wakipata huduma toshelevu ya maji.

# WATUMISHI MWAUWASA WANOLEWA



Watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA ) wanahudhuria mafunzo Maalum (Young Water Professionals) ambayo yanakusudia kuwajengea uwezo Watumishi vijana katika sekta ya maji ili kuimarisha utendaji kazi pamoja na utoaji huduma bora.



Mafunzo hayo ya siku mbili yanafanyika katika ukumbi wa City Link - Buswelu yakijikita kujenga uelewa katika masuala ya mawasiliano kazini, Uongozi, kujitambua na kuboresha mahusiano kazini pamoja na namna ya kuendana na mabadi liko.

Akifungua mafunzo hayo Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA Ndugu, Neli Msuya amesema dhamira ya mafunzo hayo ni kuleta mabadiliko kwa Watumishi na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi ili kufanikisha dhima ya kutoa huduma kwa wananchi.

Mafunzo hayo yanatolewa Kwa ushirikiano na Wataalam kutoka Shirika la Maji la Uholanzi - Vitens Evides International (VEI).

# NUKUU SEKTA YA MAJI

"Ni wajibu wetu kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata huduma ya majisafi na salama kwa wakati, tunachotakiwa ni kusimamia miradi ikamilike kwa wakati.



ENG, MWAJUMA WAZIRI

KATIBU MKUU WIZARA YA MAJI

# RC MTANDA AISIFU MWAUWASA KWA UTEKELEZAJI WA MIRADI INAYOENDELEA

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Said Mtanda amepongeza jitihada za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kwa kuendelea na jitihada za kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi.





Aliyasema hayo Julai 15, 2024 akiwa katika Kata ya Igoma Wilayani Nyamagana wakati wa mkutano wake wa kusikiliza na kuzipatia ufumbuzi kero za wananchi wilayani humo

Ninakupongeza Mkurugenzi wa MWAUWASA, Ndg. Neli Msuya kwa kutueleza bayana namna ambavyo Wizara ya Maji kupitia MWAUWASA ilivyojipanga kuboresha mitandao ya maji kupitia miradi mbalimbali uliyotueleza katika hadhara hii," amesema Mhe. Mtanda.

Awali Mkurugenzi wa MWAUWASA akiwasilisha taarifa ya mipango ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji alisema Mamlaka imejipanga kuhakikisha huduma ya maji inaimarika hususani katika maeneo ya pembezoni ambayo yamekuwa na changamoto.

"Mamlaka inaendelea na utekelezaji wa miradi ya haraka, ya muda wa kati na miradi ya muda mrefu ili kutimiza dhamira ya Serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe. Dr. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo ya maji kicwani" alisema.

Ndg. Neli alisema utekelezaji wa miradi ya muda mfupi imelenga kupunguza upungufu wa maji katika baadhi ya maeneo ikuwemo kutanua mfumo wa usambazaji maji na kwamba hivi karibuni Mamlaka itaanza ujenzi wa matenki makubwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo Buhongwa, Nyamazobe, Fumagila, Kisesa na usagara.

# MRADI WA MAJI KISIWA CHE BEZI KUNUFAISHA WANANCHI 6378



WANANCHI elfu 6,378 waishio Katika Wilaya ya Ilemela kwenye Kisiwa cha Bezi Mkoani Mwanza wanatarajia kunufaika na mradi wa maji wa kisiwa cha Bezi ambao unatarajiwa kuanza kutekelezwa mwezi septemba 2024

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri wa Wizara ya Maji Mhandisi Kundo Mathew alipotembelea na Kukagua Maandalizi ya kuanza kwa ujenzi wa mradi huo wa maji unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) ambapo ujenzi wake unatarajiwa kuanza Mwezi Septemba 2024 na kukamilika mwezi februali 2025.

Mhandisi Kundo ameeleza kuwa kazi zitakazofanyika katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa vituo 15 vya kuchotea maji, ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji la lita 250,000 na

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Ilemela Dkt. Angelina Mabula ameishukru Serikali kwa kuanza utekelezaji wa mradi huo na kusema kwamba mnamo tarehe 22 Aprili, 2024 aliuliza swali la nyongeza bungeni kwa Wizara ya Maji kuwa Lini, Serikali itapeleka huduma ya majisafi na salama kwenye kisiwa

# SERIKALI KUWEZESHA UPANUZI WA MRADI WA MAJI BUTIMBA AWAMU YA PILI

Naibu Waziri wa Wizara ya maji Mhandisi Kundo Mathew amesema Serikali kupitia Wizara ya maji itaendelea kuwezesha utekelezaji wa miradi ya sekta ya maji Mwanza ili kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi

Ameyasema hayo alipotembelea mradi wa maji wa Butimba Julai 27, 2024 na kujionea ufanyaji kazi na ufanisi wa mradi huo ambapo ameielekeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kutunza chanzo hicho na kuharakisha taratibu za kuwezesha utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa chanzo hicho ili kuongeza uzalishaji wa maji kutoka Lita Milioni 48 kwa siku hadi Lita Milioni 144 Kwa siku.

Aidha amebainisha kuwa Wizara ya Maji chini ya Waziri Mhe Jumaa Aweso ina nia ya dhati ya kutaka kufanikisha azma ya Serikali ya kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi



Amesema Mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano na Wadau wa maendeleo ambapo Mhandisi Kundo amesema ni matokeo ya Jitihada za kidiplomasia anazofanya Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan ambazo zinaimarisha mahusiano na mataifa na taasisi za kifedha za kimataifa.



Kukamilika kwa utekelezaji wa mradi huo kutaongeza uzalishaji na hivyo kutosheleza ongezeko la watu linaloendana sambamba na ongezeko la mahitaji na maendeleo ikiwemo

# MBUNGE WA ILEMELA DKT. MABULA AZURU BANDA LA MWAUWASA NANENANE 2024




Maonesho ya Wakulima (Nanenane) kwa mwaka 2024 yanaendelea katika viwanja vya maonesho Nyamhongolo ambapo MWAUWASA ni moja kati ya Wadau wanaoshiriki maonesho hayo.

Wananchi na Wadau mbalimbali wameendelea kufika na kujifunza masuala mbalimbali kuhusu huduma za MWAUWASA, miongoni mwa waliofika kutembelea Banda la MWAUWASA ni pamoja na Mbunge wa Jimbo la Ilemela Mhe. Dkt. Angeline Mabula

Kaulimbiu ya maonesho ya Nanenane kwa mwaka huu wa 2024 inasema "Chagua Viongozi bora wa Serikali za mitaa kwa maendeleo endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi".

MWAUWASA inaendelea kuwakaribisha wananchi wote kufika katika Banda Lake la maonesho ili kujifunza mengi kuhusu huduma zake.

# Zingatia Kanuni za Usafi wa Mazingira




- Epuka utiririshaji ovyo wa Majitaka.
- Tumia njia sahihi za uondoshaji Majitaka kwa kutumia magari maalum ya **MWAUWASA** kwa gharama nafuu.

**Piga Simu Bure** **0800110023**

# AGIZO LA NAIBU WAZIRI WA MAJI STONE TOWN – BUSWELU LATEKELEZWA KWA WAKATI

Naibu Waziri wa Wizara ya Maji Mhandisi Kundo Mathew ametembelea eneo la Stone Town - Buswelu Wilayani Ilemela na kukagua utekelezaji wa agizo la kuwaunganishia huduma ya Majisafi wananchi wa eneo hilo ndani ya siku kumi na nne (14), alilolitoa kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) tarehe 26, Julai 2024 alipofanya ziara na kuzungumza na wananchi wa kata ya Buswelu.

Mhandisi Kundo akiwa eneo hilo ameshuhudia nyumba kadhaa zikiwa tayari zimeunganishiwa huduma ya maji na huku zoezi la kuwaunganishia huduma wananchi likiendelea kutekelezwa na Mafundi wa MWAUWASA.



Aidha, Mhe Kundo amemshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha za miradi ya maendeleo hususan miradi ya maji ambayo kimsingi inachangia kuboresha afya na kuleta maendeleo ya kiuchumi.

Vilevile, Mhandisi Kundo amemshukuru Waziri wa Wizara ya Maji Me. Jumaa Aweso Kwa miongozo ya kuhakikisha kila Mwananchi anafikiwa na huduma ya Majisafi na Salama kama ilivyo adhma ya Mhe. Rais na kuongeza kuwa kazi ya Watumishi wa Sekta ya Maji ni kuhakikisha wanamsaidia Mhe. Waziri kutimiza majukumu aliyok abidhiwa na Mhe. Rais.

Kadhalika, Mhandisi Kundo amepongeza MWAUWASA kwa kutekeleza agizo hilo kwa wakati na kuwaeleza wananchi kuwa licha ya kuunganishiwa huduma hiyo, MWAUWASA itaendelea kutoa huduma kwa kutekeleza migao wakati miundombinu ya uzalishaji na usambazaji maji ikiendelea kuimarishwa.



Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Ilemela Mhe. Dkt Angeline Mabula amepongeza kazi inayofanywa na Serikali kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji na kuiomba Serikali kupitia Wizara ya Maji kuendelea kutekeleza miradi ya kimkakati ili kuimarisha zaidi huduma ya maji kwa wakazi wa mkoa wa Mwanza.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakazi wa eneo hilo wamepongeza kazi iliyofanyika na kutoa hamasa wa wananchi wengine kuendelea kuunga mkono jitihada hizo za Serikali Kwa kutunza miundombinu ya maji na kulipa bili za maji kwa wakati.

# UWT YASIFU UTEKELEZAJI MRADI WA MAJI BUTIMBA

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Mary Pius Chatanda amesema ujenzi wa mradi wa Maji Butimba umetekelezwa kwa ufanisi kulingana na gharama ya utekelezaji wa Mradi huo.



Ameyasema hayo Agosti 12, 2024 alipofanya ziara kwa lengo la kujionea utendaji kazi wa mradi huo ambapo ameambatana na viongozi mbalimbali wa Serikali na Chama cha Mapinduzi (CCM).



"Nimezungukia mradi huu wa kwanza na nimejionea mwenyewe nimeridhika, ni mradi mzuri na naiona Ile gharama iliyotamkwa ipo sawa sawa, Pongezi kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha uwekezaji huu na hongereni sana kwa mradi mkubwa wa aina hii" amesema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana Mhe. Amina Makilagi amesema utekelezaji wa mradi huo umekua na matokeo chanya kwa wananchi kwakuwa umeongeza wingi wa maji yanayozalishwa ikilinganishwa na

Kwa upande wake Meneja Miradi wa MWAUWASA Mhandisi Celestine Mahubi amesema mradi huo kwa sasa umetekelezwa kwa awamu ya kwanza na unazalisha Lita za maji Milioni 48 kwa siku. hapo awali.

Aidha, ameongeza kuwa MWAUWASA imejipanga kutekeleza upanuzi wa mradi huo kwa awamu ya pili ambapo itaongeza uzalishaji wa maji kufikia Lita za ujazo Milioni 144 kwa siku ukienda sambamba na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji ikiwemo ujenzi wa Matenki matano ya uhifadhi na usambazaji maji maeneo ya Kisesa, Fumagila, Nyamazobe, Buhongwa na Usagara.

# MWAUWASA YASHIRIKI KONGAMANO LA TATU LA KITAALUMA LA CHAMA CHA MADEREVA WA SERIKALI




MWAUWASA yashiriki katika kongamano la tatu la kitaaluma la chama cha Madereva wa Serikali Tanzania.

Kongamano hilo limefanyika katika Ukumbi Mikutano wa Kimataifa AICC jijini Arusha tarehe 19 hadi 23 Agosti, 2024.

Mgeni rasmi wa Kongamano hilo Mhe. Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tan zania.

Aidha kongamano hilo limeambatana na Mafunzo Maalumu kwa Madereva ili kuongeza uelewa katika utendaji wao wa kazi kutoka chuo cha usafirishaji cha Taifa (NIT), Mafunzo ya Usalama barabarani kutoka Jeshi la polisi, Maadili ya utumishi wa umma kutoka tume ya maadili, afya ya akili, mfuko wa fidia mahara pa kazi (CWF) na Toyota kwa ajili ya kujua matumizi ya magari ya kisasa.

Kauli mbiu ya kongamano la mwaka 2024 linasema “Dereva wa Serikali jitambue, timiza wajibu, usalama unaanza na wewe.

# ZAHANATI YA BULALE KATA YA BUHONGWA YAKUMBUKWA

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) imekabidhi Pampu ya chini ya maji (Submersible Water Pump) katika Zahanati ya Bulale iliyopo kata ya Buhongwa Wilayani Nyamagana.

Aidha, kifaa hiki kimelenga kuongeza ufanisi wa upatikanaji wa Maji kwa urahisi kwenda kwenye Matanki makubwa yaliyopo kwenye Zah anati hiyo.



Msaada huo uliotolewa ni sehemu ya jitihada za MWAUWASA katika kutambua na kujali uwepo na umuhimu wa makundi haya maalum.

MWAUWASA imekuwa ikichangia taasisi na makundi maalum ya Jamii kwa kutoa Matanki na vitu vingine mbalimbali ili kuwezesha kupata huduma muhimu.

# MWAUWASA YAIBUA TABASAMU KWA WAKAZI WA NANSIO – UKEREWE

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kanda ya Nansio (Ukerewe) imekamilisha zoezi la ugawaji wa vifaa vya Maunganisho Mapya na kufanikisha zoezi la kuunganishia huduma ya Majisafi Wateja wapatao 37 ndani ya mwezi Agosti 2024.









Katika Mwezi huu Agosti 2024 jumla ya Wateja 37 walioomba kuungiwa huduma ya Majisafi kutoka katika kata mbalimbali za Mji wa Nansio ikiwemo Bukongo, Nansio Mjini, Kakerege, Nkilizya, Kagera, Nakatunguru na Miti Mirefu wameunganishiwa huduma.

Akizungumzia zoezi hilo Mkuu wa Kanda ya Nansio Joseph Edward amewashukuru Wateja wote kwa kutoa ushirikiano wa dhati pindi zoezi hili lilipokuwa likiendelea.

"Ninawashukuru Wateja wote kwa Ushirikiano wenu na uvumilivu wenu, tumefanikiwa kuwaunganishia huduma ya Majisafi wateja 37 ndani ya mwezi huu, zoezi hili ni endelevu na tutaendelea kuwafikia Wateja wengi zaidi walioomba kuunganishiwa huduma na kukamilisha taratibu zote". Ameeleza ndugu Joseph

Sambamba na zoezi hilo, Wateja wamepatiwa elimu juu ya utunzaji Miundombinu ya maji, Matumizi sahihi ya maji, Malipo ya ankara, njia za Mawasiliano pamoja na huduma zingine zinazotolewa na MWAUWASA.

# MRADI WA DHARURA SAHWA- BUHONGWA MBIONI KUKAMILIKA



Utekelezaji wa mradi wa dharura wa Maji unaohusisha ulazaji wa bomba la inchi 12 Kwa urefu wa Kilomita 4.5 kutoka tenki la maji Sahwa kwenda eneo la Buhongwa umefikia hatua nzuri na unaelekea kukamilika.

Akiwa eneo la utekelezaji wa mradi huo Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA Neli Msuya amesema kwa sasa kazi inafanyika usiku na mchana ili kuhakikisha huduma inawafikia wananchi ndani ya muda uliopangwa.

Aidha, katika hatua nyingine Mkurugenzi Neli ameishukuru Serikali kwa kuendelea kutoa miongozo na kuwezesha utekelezaji wa miradi inayolenga kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi.

"Utekelezaji wa mradi huu unatumia Fedha kutoka Serikali kuu, kwahivyo tunamshukuru sana Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutuwezesha kutekeleza miradi hii, lakini pia Waziri wetu wa maji Mhe. Jumaa Aweso kwa miongozo yake ambayo imekua ikituhimiza kufanya kazi kwa bidii ili wananchi wapate huduma kwa utoshelevu" ameongeza.




Kwa upande wake Msaidizi wa Mkuu wa Kanda ya MWAUWASA Nyegezi upande wa Ufundi Mhandisi David Katakweba amesema utekelezaji wa mradi huo utakaozalisha wastani wa Lita za maji Milioni 8 kwa siku, kwa sasa umefikia zaidi ya asilimia 85.

ambapo kazi ndogo iliyobaki ya kuunganisha na kufukia bomba kwa urefu wa takribani mita 100 inatarajiwa kukamilishwa ndani ya muda mfupi ili wananchi wapate huduma katika muda uliopangwa ambao ni ndani ya mwezi huu wa Septemba.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti Madiwani wa kata za Buhongwa, Lwanhima na Mkolani zitakazonufaika na mradi huo wameshukuru Serikali kwa utekelezaji wa mradi huo na kuongeza kuwa wananchi wanayo matumaini makubwa ya huduma kuimarika baada ya mradi huo kukami lika.

Kukamilika kwa mradi huo unaogharimu TZS Millioni 860 kutaongeza wingi wa maji yanayowafikia wakazi wa kata za Buhongwa, Lwanhima na Mkolani na hivyo kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa maeneo hayo yaliyokua yakipata huduma isiyo toshelevu ya maji.

# MD MWAUWASA AWATIA MOYO MAFUNDI WANAFUNZI



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA Neli Msuya akiwa katika picha ya pamoja na Mafundi wanafunzi (wasichana) waliokuwa wakishiriki katika kazi ya kukamilisha utekelezaji wa mradi wa maji wa dharura Buhongwa.

Mkurugenzi Neli amewaasa kufanya kazi kwa bidii weledi na kuwa wadadisi wakati wakiwa katika mafunzo ya vitendo kazini.

Baada ya kazi za ufundi zilizohusisha Uunganishaji wa bomba la inchi 12 kutoka Kituo cha kusukuma maji Sahwa kwenda Buhongwa kukamilika, mradi huo umenza kufanyiwa majaribio yakuanza kusukuma maji Jana Septemba 08 ambapo Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso aliwasha mitambo ya kusukuma maji rasmi katika Kituo cha Sahwa kwenda eneo la Buhongwa.

# NAIBU KATIBU MKUU WIZARA YA MAJI AZINDUA KAMPENI "MWAUWASA MTAA KWA MTAA"

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Ndg. Agnes Kisaka Meena, alifanya ziara ya kutembelea Mtaa kwa mtaa Septemba 11, 2024 kata ya Buhongwa ili kujiridhisha na hali ya upatikanaji wa Maji na pia kuzungumza na viongozi akiwa na lengo la kuhakikisha dhamira ya Serikali ya awamu ya sita ya kuboresha huduma za maji inatekelezwa.

"Dhamira na malengo ya Rais Dk.Samia Suluhu Hassan ni wananchi kupata maji safi, hivyo tunapita kuangalia na kufanya tathmini kuona ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maji,"alisema Naibu Katibu Mkuu.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Ng'ashi Ndugu Thomas Simon ameshiriki katika Ziara hiyo iliyofuatia utekelezaji wa mradi wa maji wa Sahwa - Buhongwa ili kujiridhisha na ufanisi wake na kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi.

"Kiu ya wananchi wa Buhongwa ni maji, ndio kilikuwa kilio chao na agenda kubwa,kwa mradi huu wa dharura tangu juzi wamepata,majitunaishukuru sana Serikali, " alisema

Naye Kaimu Mganga Mfawidhi wa Kituo cha fya Buhongwa, Dkt Lightness Masito aliipongeza serikali ya awamu ya sita kwa kuondoa uhaba



"Tulihitaji maji ya kutosha kwa usafi na matumizi mbalimbali ya huduma na kwa usalama wa wagonjwa ukizingatia Buhongwa ni kituo cha afya kilicho jirani na soko, ni faraja kuona huduma hiyo imetufikia kwa wakati sasa," alisema Daktari

Kaimu Mkurugenzi wa MWAUWASA, Bi. Neli Msuya alisema "maji yalikuwa ni tatizo kubwa katika Jiji la Mwanza na maeneo ya pembezoni ikiwemo Buhongwa,hivyo tuliahidi kufanya kazi usiku na Mchana kutekeleza mradi wa Matokeo ya Haraka ambapo sasa majaribio yataendelea kwa siku tano ili kuangalia uimara wa mfumo mzima.

Aidha Neli alishukuru ujio wa Naibu Katibu Mkuu katika ziara yake ya kutembelea miradi mbali mbali na kufanya ziara ya kutembelea mtaa kwa mtaa ili kukagua hali ya upatikanaji maji na kuzungumza na baadhi ya Viongozi na Wakazi wa maeneo yaliyolemgwa na mradi huo.

# MWAUWASA YAIBUKA MSHINDI WA PILI FAINALI MAJICUP 2024



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) imeibuka mshindi wa pili katika Fainali za Mashindano ya Kombe la Maji #MajiCup 2024, yaliyofanyika Jijini Dodoma. Katika mchezo wa fainali ya mpira wa miguu, MWAUWASA ilipoteza mchezo kwa kufungwa goli 1-0 na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Zanzibar (ZURA).

Hata hivyo, MWAUWASA imeonyesha mchezo mzuri wenye nidhamu na umahiri mkubwa kwa kufika hatua ya fainali pasipo kupoteza mchezo wowote katika Mechi za Mpira wa Miguu tangu kuanza kwa Mashindano hayo mwaka huu 2024.



Mashindano hayo ya #MajiCup yalikusanya timu kutoka Taasisi mbalimbali zinazohusika na huduma ya Maji kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, yakilenga kuimarisha mshikamano na ushirikiano kati ya watumishi wa sekta ya Maji pamoja na kupeleka ujumbe kwa Jamii kuhusu Kampeni ya Udhibiti wa upotevu wa Maji na Kulinda Miundombinu na Vyanzo vya

# KAMATI YA UKAGUZI YA BODI YA MWAUWASA YATEMBELEA KANDA ZA MWAUWASA

Kamati ya Ukaguzi ya Bodi ya Wakurugenzi Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) imefanya ziara ya kutembelea kanda za Ngudu, Magu, Misungwi na Nansio- Ukerewe Sep temba 13-14, 2024.



Lengo la Ziara hiyo ni kukagua Miradi mbalimbali kujionea utendaji kazi katika kanda , kukutana na watumishi kwa lengo la kufahamiana zaidi na kuwasikiliza kwa lengo la . kuboresha utendaji kazi.

Aidha Ziara hiyo iliongozwa na Mwenyekiti wa kamati ya Ukaguzi Bi. Mwambure Ilhuya ambaye amezipongeza kanda hizo kwa jitihada zinazoendelea kufanyika za uboreshaji wa upatikanaji wa huduma ya Maji kwa wakazi wa miji hiyo.

“Nitoe wito kwa Wakuu wa Kanda kuhakikisha mnaongeza ushirikiano na wafanyakazi pamoja na viongozi katika maeneo yenu ya kanda. Kutaneni, kaeni vikao kadri mtakavyopata nafasi badilishaneni mawazo na uzoefu, naamini mkishirikiana vyema itasaidia kuboresha utoaji wa huduma ya Maji na usafi wa mazingira kwa wakazi wa maeneo yote yanayohudumiwa na mwisho wa siku Wizara na MWAUWASA itaonekana kutimiza malengo ya Serikali. ameeleza Bi Mwanabure.

Katika Ziara ya Kamati ya Ukaguzi, Mwenyekiti wa kamati ameambana na Bi. Hellen Bogoye, Lussingi Sitta, Phillipina P Labia na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mwauwasa ambaye ni Katibu wa Bodi ya Waku rugenzi.



# VIONGOZI KATA YA IGOMA WATETA NA MWAUWASA



Viongozi wa Mtaa wa Kakebe kata ya Igoma wakiongozwa na Diwani wa Kata hiyo Mussa Ngollo, wametembelea Ofisi za Makao makuu ya MWAUWASA na kuzungumza na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA Neli Msuya kuhusu hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo yao.

Katika kikao hicho Mkurugenzi Neli amewaeleza Viongozi hao kuhusu mipango mbalimbali ya muda mfupi, muda wa kati pamoja na mipango ya muda mrefu na ya kudumu ilivyopangwa kutekelezwa na MWAUWASA kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa maeneo hayo.

Akizungumza kwa niaba ya Viongozi hao, Diwani wa Kata ya Igoma Mussa Ngollo amemshukuru Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA pamoja na Timu nzima ya MWAUWASA kwa kuendelea kuwa karibu na jamii kwa kuwapokea na kusikiliza changamoto mbalimbali zinazowasilishwa kuhusu huduma ya maji na kuzitafutia ufumbuzi wa haraka.

# UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI KUCHOCHEA KASI YA MAENDELEO MWANZA

## WIZARA YA MAJI YAPONGEZWA

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Said Mtanda amesema utekelezaji wa miradi ya Maji iliyokamilika na ambayo ipo mbioni kuanza utasaidia kuchochea kasi ya maendeleo kwa wananchi.

Amebainisha hayo ofisini kwake Septemba 20, 2024 alipokua akizungumza na ujumbe wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (Europea Investment Bank - EIB) walioambatana na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA Neli Msuya kwaajili ya kujadili maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa LVWATSAN awamu ya pili unaotarajiwa kuanza kutekelezwa hivi karibuni baada ya taratibu muhimu kukamilika.



"Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan anahimiza utekelezaji wa miradi kwa ushirikiano na Wadau wa Maendeleo hivyo nawaahidi ushirikiano wa kutosha kutoka kwa Serikali kwakuwa miradi hii itaenda kuondoa upungufu wa huduma ya maji na hivyo kuchochea kasi ya Maendeleo kwa Wananchi" ameeleza na kuipongeza Wizara ya Maji kwa jitihada zinazoendelea.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA Neli Msuya amesema utekelezaji wa mradi huo wa LVWATSAN awamu ya pili na ya tatu unatarajiwa kuhusisha upanuzi wa Chanzo cha maji Butimba, upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya usambazaji maji pamoja na ujenzi mifumo ya majitaka kwa wakazi wanaoishi milimani na hivyo kuimarisha huduma hizo muhimu.

Kwa upande wake mwakilishi wa (EIB) Afrika Mashariki Lily Munyungi amesema EIB inajivunia ushirikiano uliopo na itaendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania kuunga mkono jitihada za Maendeleo katika kutekeleza miradi mbalimbali ya Maendeleo ikiwemo miradi ya kuboresha huduma za maji na usafi wa Mazingira Mwanza

# MWAUWASA YASHIRIKI USAFI SOKO LA MBUGANI KUADHIMISHA WIKI YA USAFI WA MAZINGIRA



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wamefanya usafi katika eneo la Soko Mbugani kata ya Mirongo Wilaya ya Nyamagana jijini Mwanza ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Wiki ya Mazingira Duniani.

Akizungumza katika zoezi hilo Afisa Maendeleo ya Jamii kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) Bi.Judith Mtui amesema ili kuhakikisha jamii inakuwa na Mazingira Safi ni jukumu la kila mmoja kuwa mstari wa mbele katika kutokomeza uchafu hususani hususani ule wa plastik pamoja na taka ngumu kwani kwa kiasi kikubwa ndiyo umeonekana kukithiri katika jamii.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Masoko Makuu ya Mwanza Ndg. Hamadi Chora amewasihi Wananchi kujiepusha na utupaji taka ovyo katika maeneo mbali mbali ili kuweka Mazingira salama kwa afya ya jamii na kuepukana na milipuko ya magojwa kama vile vipindupindu.

# MWAUWASA NA VEI ZAUNGANISHA NGUVU, KUPAMBANA NA UPOTEVU WA MAJI

Katika kuendelea kuhakikisha huduma ya maji Jijini Mwanza inazidi kuimarika Shirika la Maji la Uholanzi (Vitens Evides International - VEI) imekabidhi vyombo vya usafiri aina ya pikipiki kwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA kwa lengo la kuunga mkono jitihada za udhibiti wa upotevu wa Maji.



Zoezi hilo limefuatia baada ya VEI na MWAUWASA kusaini hati ya makubaliano (Memorandum of Understanding - MOU) hii leo Septemba 25, 2024 kuhusu ushirikiano wa pamoja katika suala la udhibiti wa upotevu wa Maji chini ya Mradi wa "Usalama wa Maji na uimara wa hali ya hewa kwa Maendeleo ya Mijini" (Green and Smart Cities - 'SASA').

Akizungumza wakati wa zoezi la makabidhiano hayo Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA Neli Msuya amesema ushirikiano huo utasaidia kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi kwa kupunguza upotevu wa maji na hivyo maji yanayozalishwa yataweza kuwafikia wananchi kwa wingi

"Vyombo hivi vya usafiri vitaenda kuwawezesha Mafundi wetu kuzunguka maeneo mbalimbali na kukagua miundombinu yetu kwa urahisi na haraka hivyo watakapobaini mivujo ama changamoto yoyote itakua rahisi kuifikia na kudhibiti kwa haraka" Ameeleza Mkurugenzi Neli.

Kwa upande wake Meneja Miradi wa VEI, Andries Van Eckeveld amesema VEI itaendelea kushirikiana na MWAUWASA kuunga mkono jitihada za udhibiti wa upotevu wa Maji kwa njia mbalimbali ikiwemo kujengeana na kubadilisha uwezo na uzoefu kwa Watumishi, usimamizi wa mita za maji pamoja na mambo mengine yanayosaidia kudhibiti upotevu wa Maji yanayozalishwa

Mradi wa Green and Smart Cities 'SASA' umeanza kutekelezwa mwezi Juni 2024 na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba 2026 ukihusisha masuala mbalimbali ikiwemo Usafi wa Mazingira na Maboresho ya huduma ya Maji kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ) ukitekelezwa katika mikoa ya Mwanza, Tanga na Pemba.

# WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA YAANZIA MTAA KWA MTAA





Katika kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Mteja ambayo imeanza rasmi leo (07-11 Oktoba 2024), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) imeanza maadhimisho hayo kwa kutembelea wateja wake Mtaa kwa Mtaa kwa lengo la kusikiliza na kupokea maoni mbalimbali na changamoto kwa lengo la kuboresha huduma.

Akiongea Meneja Huduma kwa Wateja MWAUWASA Sia Mrema amesema Wiki ya huduma kwa Mteja imeambatana na Ofa maalum ya msamaha wa tozo ya kurejeshewa huduma ( Re connection fee) kwa Wateja waliositishiwa huduma ambapo kwa kipindi hiki tozo hiyo haitakuwepo, sambamba na hilo MWAUWASA itatembelea wateja wake mtaa kwa mtaa ikiwa ni Sehemu ya kuthamini nafasi na mchango mzuri wa wateja katika kukuza na kuimarisha upatikanaji wa huduma.

Ndugu Celvin Paschal mmoja wa Wateja waliotembelewa ameeleza kufurahishwa na namna MWAUWASA inavyoendelea kukumbuka Wateja wake na kuonyesha thamani yao.

“Niwapongeze MWAUWASA kwa kufanya mageuzi makubwa kwenye utoaji wa huduma kwa ujumla, ni kazi kubwa imefanyika na sasa huduma imeimarika kwa kiasi kikubwa,” amesema ndugu Clevin

“Binafsi nimeridhishwa sana na huduma ya MWAUWASA hasa kwa upande wa huduma hata kama nimesafiri naweza pata bili yangu kupitia simu ya mkononi, pia nikiwa na shida yeyote naweza kupiga simu kupitia namba ya huduma kwa mteja na tatizo langu likashughulikiwa kwa wakati bila usumbufu wowote binafsi haya ni maboresho makubwa sana ukilinganisha na zamani,” amemalizia ndugu Clevin.

# KAMATI YA KUDUMU YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR YAUPA TIKI MRADI WA MAJI BUTIMBA

Kamati ya kudumu ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar imefurahishwa na uendeshaji wa Mradi wa Maji wa Butimba na kuipongeza Serikali kwa uwekezaji mkubwa uliofanyika.

Hayo yamesemwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Yahya Rashid Abdallah walipotembelea mradi huo kwa lengo la kujionea utendaji kazi wake

"Tumeona mengi ya kujifunza kupitia Mradi huu unaofanya kazi kwa teknolojia ya kisasa kabisa, kuanzia maji yanavyozalishwa na yanavyotibiwa. Tunaipongeza Serikali inayoongozwa na Rais wetu Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji huu mkubwa. Kwakweli ni Mradi wa kupigiwa mfano" ameeleza Mhe. Abdallah



Kwa upande wake Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar Mhe. Shaibu Hassan Kaduara (Mb) amesema Mradi huo mkubwa na wa kisasa umetekelezwa kwa ufanisi na kuongeza kuwa ni muhimu kwa Sekta za maji Tanzania Bara na Zanzibar kuendeleza ushirikiano ili kuhakikisha huduma ya maji kwa Wananchi inazidi kuimarika

Naye Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA Neli Msuya amesema ugeni huo ni heshima kwa MWAUWASA kwakuwa hatua hiyo itaongeza umoja na Ushirikiano zaidi katika kuendelea kuboresha huduma ya Maji kwa Wananchi.

"Tumefurahi kupokea ugeni huu na kwetu ni heshima kubwa. Tumewapitisha katika miradi iliyotekelezwa na kuwaeleza mipango mbalimbali aidha tumeongea mengi na yapo tuliyojifunza kutoka kwao," alisema na kuongeza kuwa pia kamati imeongozana na wataalamu mbalimbali wakiwemo kutoka Wizara yenye dhamana ya usimamizi wa maji na Mamlaka ya Udhibiti wa huduma za Nishati na Maji Zanzibar (ZURA).

"Hivyo tunaamini hii itaongeza umoja na ushirikiano zaidi" ameeleza Mkurugenzi Neli.



Viongozi hao Wanaendelea na Ziara yao ya siku mbili ambapo baada ya kutembelea Mradi wa maji wa Butimba na Mtambo wa Kuchakata Majitaka eneo la Gereza la Butimba (DEWATS), hapo kesho Watatembelea Miradi ya Usafi wa Mazingira ukiwemo

# MWENGE WA UHURU WARIDHIA MIRADI YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA MWAUWASA

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) imepongezwa kwa usimamizi mzuri wa Miradi ya maji na Usafi wa Mazingiraambayo imeleta matokeo chanya kwa wananchi.

Hayo yamesemwa na Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa Godfrey Mnzava wakati Mwenge ulipotembelea kukagua utekelezaji wa Mradi wa Chanzo cha maji cha Butimba pamoja na Mfumo wa kuchakata Majitaka eneo la Gereza la Butimba ( Decentralized Wastewater Treatment System DEWATS)



Mzava ameipongeza Serikali inayoongozwa na Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Maji kwa uwekezaji uliofanyika kufanikisha ute kelezaji wa Miradi hiyo.

"Lakini uwekezaji huu unaakisi namna ambavyo Mhe. Rais anatafuta majawabu ya changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi, wataalamu wametueleza kuwa mradi umekamilika na wananchi wameanza kupata maji hayo ndndiyo yalikua matarajio ya Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan" ameeleza.



# WAKAZI WA “IBANDA BUSISI” KATA YA KIRUMBA KUBORESHEWA HUDUMA YA MAJI

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) Kanda ya Makongoro inaendelea na maboresho ya miundombinu ya maji katika Mtaa wa Ibanda Busisi kata ya Kirumba kwa kuongeza mtandao wa bomba kwa urefu wa mita 300 na kunufaisha wakazi takribani 586 wa Mtaa huo ambao awali hawakua na miundombinu toshelevu ya maji



Akikabidhi bomba zitakazotumika kwaajili ya ulazaji wa Mtandao, Kaimu Mkuu wa Kanda hiyo Mishael Mayani amesema MWAUWASAinaendelea kuyafikia maeneo yote yenye changamoto za miundombinu ya maji kwa awamu na maeneo yote inaendelea kuyafikia maeneo yote yenye changamoto za miundombinu ya maji kwa awamu na maeneo yote yatafikiwa.

"Tunaendelea kuimarisha miundombinu katika maeneo yote yenye changamoto ya huduma, lengo ni kuhakikisha kila Mwananchi anapata huduma toshelevu ya maji kama yalivyo maelekezo ya viongozi wetu wa Wizara na dhamira ya Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan" amesema.

Kwa nyakati tofauti Viongozi wa Mtaa huo, wameshukuru kwa hatua hiyo na kutoa wito kwa wananchi kuunga mkono juhudi hizo

"Tunafurahi kuona eneo hili ambalo limekuwa na changamoto ya maji kwa muda mrefu sasa suluhu inakwenda kupatikana, Pongezi kwa Serikali inayoongozwa na Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa jitihada hizi na niombe wananchi tuwe walinzi na waangalizi wa miundombinu hii ili idumu na ilete tija" amesema Mhe. Wessa Juma Diwani wa Kata ya Kirumba.

"Kuunga mkono jitihada hizi za Serikali, wananchi wote tumejitolea kichimba mtaro na kushiriki pale tutakapohitajika ili kuhakikisha miundombinu hii inawekwa na tunaanza kunufaika nayo" ameeleza Pius Damian Mwenyekiti wa mtaa huo.

# ELIMU YA USAFI WA MAZINGIRA SHULE YA MSINGI BUTIMBA B





Ijumaa Oktoba 11, 2024 Maafisa kutoka kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano MWAUWASA walifika katika shule ya msingi Butimba "B" Jijini Mwanza na kutoa elimu ya Usafi wa Mazingira kwa Wanafunzi shuleni hapo.

Wanafunzi walipatiwa elimu mbalimbali ikiwemo matumizi sahihi ya vyoo wawapo shuleni na kuaswa kuwa mabalozi kwa watu wengine wawapo nyumbani juu ya uzingatiaji wa Kanuni za Usafi wa Mazingira.

MWAUWASA inaendelea kuikumbusha jamii kuhusu uzingatiaji wa Kanuni za Usafi wa Mazingira ikiwa ni pamoja na kuepuka utiririshaji ovyo wa Majitaka na kutotupa Takangumu kwenye Mfumo wa Uondoshaji Majitaka hasa kuelekea kipindi cha Mvua ili kuepusha uwezekano wa kutokea kwa Magonjwa ya mlipuko.

# ZIARA YA BODI YA WAKURUGENZI KUWASA

Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Menejimenti ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama (KUWASA) imetembelea Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kwa lengo la kuvuna ujuzi na kubadilishana uzoefu katika masuala mbalimbali

Katika ziara hiyo, KUWASA imetembelea vyanzo viwili vikuu vya uzalishaji maji Jijini Mwanza vya Capripoint na Butimba na kujionea namna shughuli za uzalishaji maji zinavyofanyika kuanzia Mwanzo hadi hatua ya mwisho ya kusambaza maji yaliyokwisha tibiwa kwenda kwa Wateja (Wananchi).



Akizungumza kwa niaba ya Bodi ya KUWASA, Mwenyekiti wa Bodi hiyo Stewart Mathias Bulaya amepongeza uwekezaji uliofanywa na Serikali hasa katika matumizi ya Teknolojia inayoendesha mitambo ya chanzo cha maji Butimba.



Ugeni huo umepokelewa na Bodi pamoja na Menejimenti ya MWAUWASA ambapo akizungumza kwa niaba ya Bodi ya MWAUWASA Mjumbe wa Bodi Ellen Bogohe amesema ushirikiano huo ni muhimu na kwamba MWAUWASA ipo tayari kuendelea kubadilishana uzoefu na Mamlaka zingine ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora kama ilivyo Nia ya Serikali na Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan.

Baada ya kutembelea Miradi ya Majisafi, hapo kesho KUWASA itapata nafasi ya kutembelea Miradi ya Usafi wa Mazingira inayosimamiwa na MWAUWASA.

# ZIARA YA WANAFUNZI MWAUWASA KUJIFUNZA KUHUSU UZALISHAJI MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA



Wanafunzi wa Shule ya Msingi "Pope John Paul II Memorial" iliyopo Nyamongo Wilayani Tarime Mkoani Mara, wamefanya Ziara ya mafunzo Mamlaka ya majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza ( MWAUWASA ) kwa lengo la kujifunza masuala mbalimbali kuhusu Uzalishaji maji na Usafi wa Mazingira.

Katika ziara hiyo Wanafunzi hao wametembelea Chanzo cha uzalishaji Maji Capripoint na Mradi wa kutibu majitaka uliopo eneo la Butuja (Saba Saba).

Wakiwa katika Chanzo cha maji Capripoint, wamejionea hatua za uzalishaji maji kuanzia hatua ya kwanza maji yanavyochukuliwa Ziwani na kupitia hatua za tiba kabla ya kuwafikia wananchi.

"MWAUWASA inahakikisha kuwa, Maji yanayowafikia Watumiaji yanakidhi viwango vya ubora vinavyohitajika kwa ajili ya matumizi ya Mwanadamu, katika Chanzo hiki maji hupokelewa kutoka ziwani na kupitia hatua zote za kuyatibu na mwisho yanapimwa kuhakiki ubora" ameeleza Bi Nebu Eliud Mtaalam wa Maabara ya Ubora wa Maji MWAUWASA.

Wakiwa katika Mradi wa kutibu Majitaka eneo la Butuja wanafunzi hao walioambatana na Walimu wao wameelezwa kuhusu mchakato wa ukusanyaji Majitaka katika Jiji la Mwanza hadi kufikia katika Kituo hicho ambapo hutibiwa katika hatua ya mwisho.

"Kwa Mwanza Majitaka hukusanywa na kusafirishwa kupitia vituo vitatu vilivyopo Makongoro, Kirumba Na Mwanza South na kisha kufika kwenye Mabwawa haya 17 kwaajili ya mchakato wa kuyatibu." Ameeleza Bi. Vivien Temu Kaimu Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano Uhusiano MWAUWASA

Kwa niaba ya ugeni huo, Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo Mwl. Eutropia Ngeleck ameshukuru kwa ziara hiyo ya Mafunzo na kwamba itaenda kuongeza chachu ya Wanafunzi hao kuendelea kusoma kwa bidii na kufikia Malengo



# JELA MIAKA MITANO KWA KUMJERUHI MTUMISHI WA MWAUWASA



Mahakama ya Wilaya ya Nyamagana Mkoani Mwanza imemhukumu Kifungo cha miaka mitano jela RAMADHANI JUMA Mkazi wa kata ya Kishiri Wilaya ya Nyamagana Jijini Mwanza kwa kosa la shambulio la kudhuru mwili kwa kumpiga spana na kusababisha kuvunja mfupa wa mguu wa Bw. MANYILI RICHARD DENNI Mtumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), wakati akitekeleza majukumu yake ya kusitisha huduma ya maji mnamo tarehe 15 Julai 2022 baada ya kubaini kuwa Mteja huyo amejirejeshea huduma pasipo halali.

Hukumu hiyo ilitolewa na Mheshimiwa Hakimu Mkazi Mkuu Juma Mpuya, mnamo tarehe 13 Juni 2024 baada ya kusikilizwa kwa kesi hiyo, ambapo ilimtia Mtuhumiwa hatiani chini ya kifungu cha 241 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura Na.16 iliyorejewa Mwaka 2022 na kwamba kupitia adhabu hii litakuwa funzo kwake na kwa watu wengine wenye tabia kama hiyo.

Katika hatua nyingine, Kitengo cha Sheria cha MWAUWASA kimetoa ushauri zaidi kwa Mtumishi huyo ikiwa ni pamoja na kufungua shauri la madai dhidi ya mteja huyo, ili kudai fidia kutokana na hasara, mateso au majeraha aliyoyapata katika kadhia hiyo. MWAUWASA inatoa rai kwa wateja wake na wananchi kwa ujumla kuendelea kushirikiana na Watumishi pindi wanapopita kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria.

# MWAUWASA YAWANOA WANAFUNZI WA SAHARA NA MWENGE KUHUSIANA NA USAFI WA MAZINGIRA

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza ( MWAUWASA ) imetoa elimu kuhusu faida na namna bora ya kuzingatia Usafi wa Mazingira ikiwemo kutunza miundombinu ya vyoo ili kusaidia kujilinda na Magonjwa ya milipuko.

Elimu hiyo Imetolewa kwa Wanafunzi wa shule ya Msingi Sahara iliyopo kata ya Pamba Wilayani Nyamagana pamoja na shule ya Msingi Mwenge iliyopo kata ya Nyamanoro Wilayani Ilemela.



Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano MWAUWASA Bi. Vivien Temu ameeleza kuwa, Matumizi yasiyo sahihi na uharibufu wa miundombinu na mifumo ya Majitaka yanaweza kusababisha athari kubwa kwa jamii



“Miundombinu ya Majitaka isipotunzwa na kutumika kwa usahihi husababisha kuziba kwa chemba na mifumo ya Majitaka jambo ambalo hupelekea uharibifu wa Mazingira na mlipuko wa Magonjwa ya kuambukiza,”

Nae Mwalimu Wilson Kunju ameishukuru MWAUWASA kwa kutoa elimu hiyo na kusisitiza kuwa Wanafunzi wanatakiwa kuwa mabalozi kwa kufikisha elimu hii kwa wanafunzi wenzao na jamii wanayoishi.

“Elimu ya utunzaji wa Mazingira hasa Majitaka imekuja kwa wakati sahihi na ni elimu inayopaswa kurithishwa, kwa kuanzia na hawa Wanafunzi wadogo kunawasaidia kujiejengea tabia endelevu na kuchukua majukumu ya utunzaji wa Mazingira. Mkawe mabalozi wema katika hili mkiwa nyumbani na hata Shuleni,” ameeleza Mwl. Kunju

MWAUWASA inaendelea kuwasisitiza Wananchi kuzingatia kanuni za Usafi wa Mazingira hasa kipindi hiki cha Mvua ili kuepusha uchafuzu wa Mazingira unaoweza kuhatarisha

# MWAUWASA NA NEMC KUSHIRIKIANA UHIFADHI WA MAZINGIRA




Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) Neli Msuya, ametembelea Ofisi za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Jijini Dar es Salaam kwaajili ya majadiliano kuhusu uhifadhi wa Mazingira katika uwekezaji wa miundombinu ya usam bazaji maji Mkoani Mwanza.

Katika Ziara hiyo, Mkurugenzi Neli amepokelewa na kufanya majadiliano na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Lilian Lukambuzi ambapo majadiliano hayo yalijikita katika kubadilishana uzoefu na kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji.

# SEKTA YA MAJI MWANZA NA WIZARA WAJADILI UTEKELEZAJI WA MIRADI YAKIMKAKATI

Sekta ya Maji Mkoa wa Mwanza ikijumuisha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), RUWASA Mkoa wa Mwanza, Bodi ya bonde la ziwa Victoria pamoja na Maabara ya maji Mkoa wa Mwanza, wamekutana kujadili kuhusu utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayolenga kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Mkoa wa Mwanza.

Mkutano huo uliowakutanisha Wawakilishi kutoka Wizara ya Maji pamoja na Viongozi na Wataalam wa Sekta ya maji Mwanza umelenga kujadili tathimini ya utekelezaji wa miradi hiyo ikiwa ni pamoja na Mradi wa kimkakati wa Visima 900 unaotekelezwa ili kuwafikia wakazi wa maeneo yasiyofikiwa na huduma ya maji.

Mbali na mradi wa kimkakati wa Visima 900, miradi mingine ya kimkakati iliyojadiliwa ni pamoja na miradi ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji katika maeneo mbalimbali mkoani Mwanza inayotekelezwa na MWAUWASA, RUWASA Mkoa wa Mwanza pamoja na Bodi ya maji bonde la ziwa Victoria

Aidha, katika Mkutano huo Sekta ya Maji Mkoa wa Mwanza imewasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo ya kimkakati kwa Wawakilishi wa Wizara ya Maji na kubainisha mafanikio na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa miradi ili changamoto hizo ziweze kupatiwa ufumbuzi na kufanikisha utekelezaji wa miradi hiyo inayotarajiwa kuleta matokeo chanya kwa wananchi wengi zaidi.



# UKAGUZI MIUNDOMBINU YA MAJITAKA



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) Bi. Neli Msuya amefanya ziara ya kutembelea na kukagua Miundombinu ya Usafi wa Mazingira maeneo mbalimba



Ikiwa ni pamoja na Kituo cha uondoshaji Majitaka Mwaloni, Mjini kati na Kituo cha Mwanza kusini (Mwanza South). Lengo likiwa ni kukagua ufanisi wa Miundombinu hiyo ili kujiandaa na Mvua za Masika zilizoanza kunyesha.

Amefanya ziara hiyo tarehe 03 Desemba, 2024 akiwa ameambatana na Kaimu Meneja wa Usafi wa Mazingira Mhandisi Wilbert Bujiku pamoja na wataalam wa MWAUWASA.

Aidha MWAUWASA inaendelea kuwasiliana kwa karibu na Mamlaka husika ikiwemo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Ofisi za Halmashauri lengo likiwa ni kushirikiana na kutoa elimu ya usafi wa mazingira kwa wananchi.

Katika ziara hiyo fupi pia alikutana na madereva wa magari ya uondoshaji wa majitaka, kuzungumza nao na kuwakabidhi mipira ya unyonyaji wa majitaka ikiwa ni jitihada za Mamlaka kuimarisha huduma hiyo

# MWAUWASA
## KIDIJITALI




**Tembelea tovuti yetu**

www.mwauwasa.go.tz

Pata taarifa muhimu kupitia mitandao yetu ya kijamii

**Mwauwasatz**